RAIS MOI akimpongeza mmoja wa machifu walio zawadia heshima ya kitaifa kwa kazi yao bora katika ikulu ya Nairobi hivi karibuni.

PICHA: KENYA NEWS AGENCY

TWAISHUKURU SERIKALI KWA NYONGEZA

WAFANYI KAZI wa Serikali pamoja na walimu nchini Kenya, wana kila sababu ya kufurahia nyongeza mpya za mishahara, malipo ya nyumba pamoja na marupurupu mengine. Muheshimiwa Rais Moi aliweka sahihi katika mapendekezo hayo ya Waruhiu siku ya Alhamisi, na ikatangazwa kutoka Ikulu kwamba malipo hayo mapya yataanza kulipwa kuanzia tarehe mosi mwezi wa Oktoba, mwaka huu. Sasa wafanyi kazi wangojea kutekelezwa kwa amri hiyo.

Mara ya mwisho walimu kupata nyongeza, ilikuwa ni mwaka wa 1977. Kuanzia wakati huo hadi hivi sasa, bidhaa kwa jumla zimepanda bei mara kwa mara na baadhi ya biadhaa kama petroli, imepanda bei zaidi mara tatu. Nauli za magari zimepanda bei sana hivyo imekuwa vigumu kwa mwalimu kuweza kusafiri siku za likizo akenda kujipumzisha kikamilifu akijiandaa kwa kazi mpya mwaka unaofata.

Sasa serikali yetu imefikilia uamuzi wa kutoa nyongeza ili kila mfanyi kazi afanye kazi kwa bidii akijua kwamba na yeye ataweza kufurahia maisha baada ya kazi. Lakini tuna imani kwamba wafanyi kazi wetu kwa vile wao ni watu wa busara na wengi wao ni watu waliosoma vizuri, watafanya juu chini ili nyongeza hizo zifanyiwe kazi ya maana sana, kwani ni pesa inayokuja baada ya kumwaga jasho jingi sana.

Kelele nyingine za mfanyikazi ni nyumba. Serikali imekubali pia kutoa nyongeza katika malipo ya nyumba, kwa vile inaelewa fika shida ya kupata maskani hasa katika miji mikubwa. Lakini pia nyongeza hiyo iwapo itakwenda katika mifuko ya matajiri na wenye majumba kila mwezi na kila mwaka bila ya wafanyi kazi kuibuka na kutafuata namna ya kuanza kusimamisha nyumba zao, basi kilio hichi hakitafika mwisho.

Wafanyikazi kwa ujumla ni budi wajiunge na vyama vyao vya Ushirika na Mikopo ambavyo takriban vimeenea katika idara zote, wachukue mikopo ya maana na waanzishe nyumba zao wenyewe kwa haraka kama inavyowezekana. Ni aibu kubwa iwapo nyongeza hizi zitakwenda kwenye vilabu vya pombe. Wakenya lazima wafahamu kwamba sasa ule wakati wa kuchezacheza na pesa umekwisha. Pesa zinakuja kwa njia ngumu kwa hivyo zitumike kwa njia nzuri.

GARI YA Abiria ya matatu kigongana na gari ndogo karibu na daraja lipya la Nyali wakati taa za kuongezea magari zilipo harabika ghafla hivi majuzi. Picha hii yaonyesha watu wakiizunguka gari la matatu lilihusika na ajali hiyo.

PICHA: ALI WARSHOW

GAZETI la *COASTWEEK* latoa Mualiko kwa akina mama na wasichana kujitokeza Uwanjani na kutoa maoni yao kuhusu shughuli mbali mbali za ujenzi wa Taifa.

Kila maelezo yataje sehemu ya kuzaliwa, malunzo, umri, kazi na mapendeleo ya aina gani katika maendeleo ya akina mama kwa jumla. Maelezo yote yafuatane na picha. Maelezo na picha zikitumiwa mshindi atapatiwa zawadi muruwa.

Lete maelezo na picha ya sura yako kwa kutumia address ya *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya.

Tutapokea washikiri kutoka kote bara la Afrika na Visiwani, Malagasy, Comoro, Mauritius, Unguja na Pemba, Sheli Sheli na kadhalika.

Harambee ya Ujamaa Social Club yafana

MAMIA YA watu walihudhuria Harambee iliyofanya sana, hapo Mwembe Tanganyika, siku ya Jumapili iliyopita, ambayo ilitayarishwa na vijana wa Ujamaa Social Club na wakamualika kama mgeni wa Heshima, Naibu Msimamizi wa Banki Kuu ya Kenya, Bwana Ahmed Abdalla.

na SAID BURHAN

Katika Harambee hiyo, jumla ya shillingi 403,226/60 zilikusanywa ambapo mgeni wa heshima yaani Bw. Abdalla alileta shillingi 85,000, baada ya kwisha kutoa nasaha zake kwa uma uliohudhuria.

Alitaka watu wote wawe na moyo wa kujenga kwani kila wilaya ina watu wakutosha wakuweza kujifanyia mambo yao wenyewe pasi na kungoja watu wengine.

Katika hotuba yake iliyoshangiriwa sana, alimsifu sana mwenyekiti wa Kanu tawi la Mombasa mheshimiwa Shariff Nassir kwa moyo wake wa ukarimu kwa popote pale aitwapo kwa kuongoza harambee.

Aliongeza kwamba, Bw. Nassir leo amekuwa mmoja kati ya viongozi ambao maneno yao huthaminiwa katika ngazi za juu kabisa za uongozi wa nchi hii, kwa sababu yeye amejifanya kwamba ni mtumishi wa watu wa Kenya nzima na siyo Mombasa peke yake.

Mwisho alisema kwamba msaada aliotoa si wa mwisho, na yeye yuko tayari kusaidia tena atakapotakiwa kufanya hivyo na wasimamizi wa jengo hilo.

Naye Waziri Mdogo wa Biashara Bw. Nassir, akihutubia katika harambee hiyo, alionya viongozi ambao kazi zao ni kupita vichochoroni wakieneza fujo baada ya kubwagwa katika uchaguzi.

Alitoa mfano wa fujo la huko bandarini Kilindini na akaonya wachocheaji hao kwamba wasipokomesha fujo hilo mara moja basi watakiona cha mtema kuni.

Bw. Nassir alithibitisha imani ya raia kwa Mtukufu Rais Moi na akasema kwamba Rais amewekwa na wenyewe wananchi kwa upendo wao na kwa hivyo wao watafata uongozi wake tu.

Mwengine aliyehutubia mkutano huo ni Meya wa mji wa Mombasa Diwani Rajab Sumba ambaye alionya vijana ambao wanajiunga na magenge ya wakora humu njini na akathibitisha kwamba vijana hawa ambao wana sumbua wananchi hawatavumiliwa hata kidogo.

BW. Abdulaziz El-Kathri

Diwani Sumba alisema kwamba wanaowaharibu vijana hawa, ni wazazi wenyewe kwa vile mara mkora afikishwapo korokoroni, mzazi wake huwaendea mbio madiwani na wabunge ili wende wakamtoe mtoto huyo. Meya alitaka wazazi wasimamishe mtindo huo na pia wasiweke silaha ya kura mbele ili kuwapa nguvu wakora hao.

Akiufungua mkutano huo, mwenyekiti wa Ujamaa Social Club Bw. Abdulaziz aliwaomba wote waliohudhuria kuchanga kwa ukarimu ili jengo hilo lao limalizike kama ilivyopangwa.

Wakati likimalizika, alisema kwamba litatoa nafasi ya skuli ya nasari kwa watoto mia moja.

Viongozi wa Ujamaa Social Club ni kama wafuatavyo — mwenyekiti: Bw. Abdulaziz El Kathiri, msaidizi wake: Mbarak M. Baadel, mwandishi: Abbas Muhsin, naibu: Patel Ali, mshika hazina: Hussein Badru, na makamo: Said Ahmed.

KWA UFUPI

Mr H. M. Nebu amewaonya wanafunzi wa Shule ya Watu Wazima kuacha vitendo vya kupika majungu badala ya kuendeleza kisomo chao.

Bwana Nebu alieleza haya baada ya kutokea mzozo katika shule ya kina mama ya Mkotachingo ambapo yeye ni mwenyekiti.

Alipongeza Mwalimu Mkuu wa Shule kwa kazi bora anayofanya.

SAUTI ZA WASOMAJI

COASTWEEK Sanduku La Posta 87270 Mombasa KENYA

K.N.U.T. yahitaji kupongezwa na walimu

NAOMBA nafasi kutoa shukurani zangu nyingi kwa Chama cha Walimu (K.N.U.T.) kwa kutayarisha mapendekezo ya nyongeza za mshahara, malipo ya nyumba pamoja na marupurupu mengine na wakayafikisha kwa kamati iliyohusika kwa kuyachunguza katika wakati unaofaa, nayo yakapitishwa na serikali yetu baada ya kufanyiwa mabadiliko kidogo tu.

Naamini sasa walimu watavuta pumzi kwani lile suala lao la siku zote lisemalo nyongeza ziwapinyongeza ziwapi sasa limejibiwa. Na yaonyesha dhahiri walimu wameshainukiliza harufu ya pesa na sasa nyimbo inayoimbwa ni kuwa pesa zaja.

Kupitia kwa gazeti hili, nawapongeza viongozi wa K.N.U.T. wa ngazi zote na mimi kwa vile ni mwalimu wa Manispaa ya Mombasa, wajibu wangu kikamilifu, ni kumuomba mwenyekiti wa K.N.U.T. tawi la Mombasa akatupelekea hongera zetu kwa viongozi wa Chama cha Walimu walioko Makao Makuu Nairobi wakiongozwa na Bw. A. A. Adongo. Huu ndio wakati mzuri wa kupeyana mikono ya furaha.

Hii ndiyo kazi ya chama kwa kupigania wanachama wake wapate haki zao. Na kwa kupitia gazeti hili hili, pia ningemuomba Afisa wa Elimu wa Manispaa ya Mombasa atayarishe jadiweli za malipo nyongeza na mshahara mpya kwa wakati unaofaa ili walimu wapatiwe malipo hayo ili baada ya miaka mitatu, washerehekee Krismasi bila ya kukopa.

Kwa furaha ya walimu, ingawa imebaki wiki moja tu kabla ya mtihani wa C.P.E. lakini nguvu za walimu za kupata pesa, watashika miti ya chaki mpaka kengele ya mwisho.

P. Es. A. Mingi,
MAGONGO.

Twajiunga na serikali kudumisha amani

NATOWA pongezi zangu kwa niaba ya Chama cha Islahil Islammiyya of Kenya na matawi yake yote yaliyoko Mkoa wa Kaskazini.

Tunazipongeza serikali mbili, Rais wa Somalia, na Rais wetu wa Kenya; kwa taarifa zao tulizozisoma.

Tuna mpongeza Mtukufu Rais Moi kwa matamshi yake ya kuipongeza serikali ya Somalia, na kuwa zitakuwa na ujirani mwema.

Chama cha Islahil Islammiyya of Kenya na Waislamu wote katika Jamhuri hii ya Kenya zinawatakia Marais wetu wawili amani, uthabiti, ujirani mwema, kwa maslaha ya nchi hizi mbili.

Natowa mwito hali ya amani, irudishwe kwa haraka sana iwezekanavyo katika mkoa wa Kaskazini, kwa sababu kama zifuatawo:

- Maendeleo yaliondeshwa mnamo 1963 hadi 1980 ni maendeleo makubwa yasiyo kiasi na hayafai kusimamishwa kwa sababu ya wachache wasiotosheka.
- Uhuru wa kuabudu uliopewa wananchi wa mkoa huo, niwaukamilifu, haufai kurudishwa nyuma.
- Uhuru wa Uchumi ni wajuu na haufai kurudishwa nyuma.
- Haki aliyopewa mwana Adamu na katiba ya nchi hii mkoa wa Kaskazini ni kama mkoa mwengine Kenya. Kwa wkati huu mimi natowa ushahidi wangu kwa ukamilifu, mia kwa mia raia wa mkoa wa Kaskazini, wazee, wanawake, vijana, ni watiifu kwa Rais Moi na serikali yake.

Na wamewalaani mbele zangu katika mikutano ya hadhara wezi na wanyanganyi, kikundi cha watu wachache wasiotosheka, na wasio kuwa raia wa nchi ya Kenya.

Nitafurahi serikali yetu tukufu irudishe amani usalama na maendeleo, na uhuru kamili wa Mwana Adamu kusudi nchi yetu iendelee mbele.

M. A. Amana,
secretary general, Islahil Islammiyya of Kenya,
MOMBASA.

Coastweek ★★

SWAHILI CROSSWORD NO. 104



KWENDA KULIA:

1. Akajua
6. Ama
7. Kituo cha matangazo
9. Umoja wa mataifa
10. Nusu ya mimi
11. Uitupe juu
14. Kiungo cha maneno
15. Kinyume cha adhibu
17. Mpuzi
19. Chagueni, tizameni

KWENDA CHINI:

1. Ghali, inayopatikana kwa taabu
2. Hufanya ule chakula sana
3. Medical Officer
4. Ndani ya ua
5. Ama
8. Asafisha
9. Huja wakati wa mvua
12. Mtungo
13. Namna ya mnyama wa mwitu
15. Kuvuta mate kwa nguvu
16. Mzoga
17. Utupiwa si watu
18. AK kama ilivyo

JEMBE

UNGA SAFI NO. 1

JINA ____

SANDUKI LA POSTA ____

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 102

[1] Alice Gem, Sanduku la Posta 80330, Mombasa,

[2] Horasi Juma, Sanduku la Posta 87478, Mombasa,

[3] Charles Musembi, Sanduku la Posta 98574, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 102 —

KWENDA KULIA:

1. MADHUMUNI, 6. AKA, 7. IMARISHWA, 9. ET, 10. IN, 11. KWAA, 12. PATE, 14. IZA, 15. HUA, 16. MSANAPITI.

KWENDA CHINI:

1. MTIRIRI, 2. HARARA, 3. UKI, 4. MASUKE, 5. NYWEA, 8. ATAMANI, 12. PAUA, 13. TOPA, 15. HOI.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 27.11.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.